



# UKWELI KUHUSU UCHANGIAJI DAMU


- Hakuna mbadala wa damu na haiwezi kutengenezwa. Damu zote zinazotumika ili kuokoa maisha zinatokana na wachangiaji kama wewe.
- Damu inayokusanywa hupimwa VVU, Homa ya ini na Kaswende.
- Utafanyiwa uchunguzi mdogo wa afya kama shinikizo la damu na wingi wako wa damu mwilini.
- Mchango wako utawasaidia wagonjwa wa saratani, waathirika wa ajali, mama na watoto.
- Siku zote damu huhitajika hospitali.
- kuchangia damu mara kwa mara husaidia kukufanya uwe mchangiaji salama iwezekanavyo! Kwa kuchangia damu, utasaidia kuhakikisha kuwa kuna damu kwa ajili yenu, watu uwapendao na mtu yeyote mwingine ambaye anahitaji.
- Kila unapochangia damu unaokoa maisha watu zaidi ya mmoja.
- HUWEZI kupata maambukizi kwa kuchangia damu, ni asilimia 100 salama.
- Ni haraka! Mchakato mzima unachukua chini ya dakika 30.
- Ni jambo zuri kuokoa maisha. Unaweza kuchangia kila baada ya miezi 3-4.
- Kuchangia damu hakuwezi sababisha madhara kwa afya yako.



## Mambo Muhimu yanayohusu Mazao ya Damu

Damu ina chembe nyekundu , chembe nyeupe , Chembe sahani na plasma;

- Chembe nyekundu za damu hubeba oksijeni katika mwili.
- Chembe nyeupe za damu husaidia kupambana na maambukizi.
- Chembe sahani huasaidia damu kuganda.
- Plasma ni kimiminika ambacho hubeba platelets, chembe nyekundu na chembe nyeupe.
- Kila sehemu ya damu yako husaidia kumpa mtu fursa katika maisha mapya.



## Sifa za mtu anaeweza kuchangia damu

- Awe na umri kati ya miaka 18-65
- Awe na uzito usiopungua kilo 50
- Asiwe na maradhi kama kisukari, shinikizo la damu, upungufu wa damu
- Asiwe mjamzito au anenyonyesha
- Asiwe na mwenendo hatarishi ambao unaweza sababisha kupata maradhi yaambukizwayo kwa njia ya damu kama Virusi vya ukimwi, homa ya ini (Hepatitis B na C) na kaswende
- Asiwe katika Tiba yoyote



**Unahofu kuja peke yako? Mlete rafiki yako!  
Uchangiaji damu ni utaratibu uliyo salama na ufanyika kitaalam.**

**Usisubiri. Okoa maisha leo!**

**Changia Damu, Okoa Maisha**